MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 1 TOLEO 2

AUGUSTI 26, 2008

KIJARIDA CHA BURE— SOMA MPE MWINGINE!

SPIKA SITTA AMUAMBIA RAIS "ONGEZA UKALI"



Rais Kikwete na Spika Sitta

Na. Fred Katunzi



Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samuel Sitta (Urambo Mashariki – CCM) siku ya Alhamisi aliamua kumtolea uvivu Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Jakaya Kikwete kwa kumuambia wazi kuwa aongeze ukali katika kusimamia nidhamu na kuhakikisha utawala wa sheria unakuwepo nchini.

Mhe. Sitta alitoa ushauri huo wa bure na wa wazi alipojibu hotuba ya Rais iliyotolewa siku ya Alhamisi Bungeni hapo. Akizungumza mara tu baada ya Rais Kikwete kuhitimisha hotuba yake hiyo maalumu ambayo ilikuwa inasubiriwa na wananchi wengi Ndg. Sitta alimwambia Rais Kikwete kuwa "wabunge wanaona pamoja na mambo makubwa yanayofanyika katika maboresho ya utumishi bado kuna ulegevu, unajidhihirisha katika ahadi zinazotamkwa na serikali bungeni na kwingineko. Bado inaonekana baadhi ya mambo hayajatekelezeka kadiri inavyotakiwa"

> **Bado kuna ulegevu unajidhihirisha katika ahadi zinazotamkwa Bungeni...**

Akiongea kama mkuu wa mhimili mwingine wa dola na ambaye hayuko chini ya Rais Spika Sitta aliendelea kwa kusema kuwa "Ni kweli tuna utawala bora lakini mizani yetu inaelekea kuelemea zaidi kutazama haki za mtu mmoja mmoja kuliko maslahi makubwa zaidi ya taifa letu. Mambo ya ovyo ovyo tokea yale ya commodity import support (cis), suala la rada na fedha za epa (akaunti ya madeni ya nje), ambayo umeizungumza kwa kirefu." Alipofikia hapo ndipo Ndg. Sitta alipochomekea na kusema "Sisi bunge tunakuahidi ukiongeza ukali kidogo, katika mambo haya....tutakuwa tayari kupokea mapendekezo yasiegemee sana kuwasikiliza sana hawa watendaji."

Maoni hayo ya Spika yaliwashangaza watu wengi ambao hawajazoea kuona hotuba ya Rais inajibiwa papo kwa papo. Watu kadhaa waliozungumza na Cheche walielezea kitendo hicho cha Spika kuwa "ni cha mfano na cha kijasiri". Bw. Fred Mugisha wa eneo la Mwaloni Mwanza ameelezea maneno ya Spika Sitta



Benjamin. G. Mwalukasa
Mhariri

Kijarida Ulichoshika

- **Kinatoka kila Jumanne**
- **Ni cha bure kabisa!**
- **Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!**
- **Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.**
- **Ni kijarida chako!**
- **Haki zote za kuchapa zimeruhusiwa!**

HOJA YA MWANAKIJIJI— HOTUBA YA RAIS IJIBIWE!

Mojawapo ya vitu ambavyo vinakomaza sana mjadala huru na kuchangia utajiri wa maoni ni uwezo wa kupata mawazo tofauti kutoka kwa watawala.

Baadhi ya watu bila ya shaka walishangazwa na wengine kushtushwa na kitendo cha Spika wa Bunge la Muungano Mhe. Samuel Sitta kuijibu hotuba ya Rais papo hapo na kusema mtazamo mwingine wa masuala ya Taifa. Ile haikuwa kawaida.

Kwa haki inapaswa kuwa jambo la kawaida kuwa endapo kiongozi wa kitaifa anahutubia kwa Taifa zima haijalishi anatoka chama gani ni muhimu kujenga utaratibu wa kujibu hoja zake papo hapo.

Nchini Marekani na baadhi ya nchi nyingine majibu hayo hutolewa na kiongozi wa Upinzani aliyechaguliwa kujibu hoja za msingi. Na hufanywa kwa muda mfupi kuliko hotuba yenyewe.

Ni vizuri basi Rais anapotoa hotuba kwa Taifa na ikarushwa na vyombo vya habari hotuba hiyo ijibiwe na majibu hayo yarushwe pia na vyombo hivyo hivyo. Vinginevyo vipigwe faini!

Ndani ya Toleo Hili

Sitta hakusita	1
Hotuba ya Rais ijibiwe	1
ATCL matatani Se. 1	2
Tujifunzi kukataa	3
Mpango unadhalilisha	3
Vikatuni na Picha	4
Kutoka Mtandaoni	4

HABARI MBALIMBALI

ATCL MATATANI (SEHEMU YA 1)

Na. Mahmoud Rashid



Shirika la ndege la Tanzania (ATCL) ambalo bado linajitahidi kutoka katika kilindi cha matatizo ya ukwasi hivi karibuni limejikuta likikabiliwa na changamoto nyingine ambazo zinatishia uhai wa shirika hilo linaloongozwa na Bw. David Mattaka.

Mambo hayo ni tishio la marubani wake kutoka Storm Aviation kutishia kusimamisha kazi kwa kutolipiwa pango Movenpick, ukosefu wa vipuri muhimu vya Boeing, na deni lao kwa Wallis Trading.

Marubani wa Storm Aviation ndio waliokodishwa na ATCL kuileta ndege ya Airbus kutoka El Salvador ilikokuwa inafanyiwa matengenezo katika "gereji" ya Aeroman nchini humo.

Kwa mujibu wa Mkataba wa ATCL na Storm Aviation kampuni yetu ya ndege ilitakiwa kuhakikisha marubani hawa wanafikia katika hoteli yenye hadhi ya nyota tano (Five Star Hotel).

Ni kutokana na kipengele hicho hoteli ya Movenpick ilichaguliwa. Hata hivyo kuanzia mwezi Juni kumekuwa na matatizo ya malipo toka ATCL kwenda Movenpick.

The Morale of our pilots is very low , this is not good!

Marubani hao wamejikuta wakikabiliwa na tishio la kutimuliwa kutoka hoteli hiyo baada ya shirika hilo ambalo limekuwa likipokea ruzuku ya mabilioni ya shilingi kutoka serikalini kushindwa kuwalipia makazi hayo na hivyo kulazimisha Storm Aviation kutishia kuwa endapo fedha za hoteli zisingelipwa basi marubani hao wangesimama kufanya kazi na ikibidi kurudi Uingereza.

Kwa mujibu wa chanzo chetu kilichoko Uingereza marubani hao wa Storm Aviation Kapt. Baker, Kapt. Krakowcyk, na Kapt. Adrian Akers Douglas walitaarifu makao makuu ya shirika hilo kuwa walikuwa na hofu ya kuondolewa kwenye hoteli hiyo ya kitalii ya Movenpick baada ya ATCL kuchelewa kulipa pango.

Kwa mujibu wa chanzo hicho siyo tu malipo ya pango ambayo yamechelewa-eshwa bali pia malipo ya mishahara ya marubani hao.

Marubani hao wamelazimika kutumia kadi zao za Kibenki (Credit Cards) kulipia vyumba vyao wakitegemea fedha hiyo kurejeshwa na ATCL. Hata hivyo kama tulivyosema hapo juu hadi wiki iliyopita ATCL ilikuwa haijakamilisha malipo hayo na kusababisha marubani hao kuendelea kutumia kadi zao hizo.

Kutokana na mkataba kati ya ATCL na StormAviation ambao Cheche imeuona shirika letu la ndege lilikodi marubani hao kuirusha ndege hiyo ya Airbus kutoka San Salvador hadi hapa nchini, na baadaye kuwa marubani wa muda katika safari za ndege hiyo katika maeneo mbalimbali ya nchi na kwenda Afrika ya kusini. ATCL lilikubali kuwagharimia kila kitu ikiwemo malazi na chakula pamoja na kulipa mishahara yao. Hadi tarehe 18 wiki iliyopita StormAviation bado walikuwa wanahangaika ili marubani wao wasiwe na wasiwasi wa wapi watakula na kulala.

Afisa mmoja wa SA aliyekataa kutajwa jina lake aliiambia Cheche kwa kimombo kuwa "our pilots morale is very low and as pilots they should not work under such a cloud of uncertainty" yaani, "mwamko wa marubani wetu umepungua sana na kama marubani hawapaswi kurusha ndege wakatika katika hali ya wasiwasi namna hiyo".

(Itaendelea wiki ijayo)

UKIMALIZA KUSOMA MPATIE MWINGINE BURE!

SPIKA SITTA (KUTOKA UK 1)

kuwa "ni ya kutia moyo kuwa baadhi ya viongozi (inaendelea) wetu wanaona kile ambacho tunakiona sisi wananchi wa kawaida".

Naye mkazi wa Ngarenaro Arusha Bi. Salma Kijo amesema kuwa alifurahishwa na na hotuba ya Rais hasa mpango wake wa kuanzisha mchakato wa kufikia uwakilishi wa asilimia 50/50 Bungeni. "Ni mpango mzuri kwani unatambua mchango wetu kina mama katika ujenzi wa Taifa na kwa hakika umechelewa kwa zaidi ya miaka 40" Alisema Bi. Kijo. Na kuhusu maneno ya Spika Sitta Bi. Kijo hakukubaliana na mtazamo wa watu wengine kuwa ilikuwa ni sawa kwa Spika kusema maneno hayo hadharani.

"Sidhani kama Spika alimtendea haki Rais kwani ile ilikuwa ni hotuba ya Rais na kama yeye Spika alikuwa na yake anataka kusema angeyatafutia wakati mwingine lakini siyo kumdharaurisha Rais miongoni mwa Watanzania namna ile" alisema dada huyo ambaye ni Mwalimu wa shule moja ya Sekondari iliyoko Moshi ambaye yuko kwenye likizo ya uzazi.

Katika hotuba yake kwa wananchi, Rais Kikwete alizungumzia kwa kirefu mafanikio ya serikali ya awamu ya nne katika miaka miwili na nusu iliyopita. Hata hivyo kiini cha hotuba yake kilizunguka katika masuala makubwa mawili ambayo wananchi walikuwa wanasubiri kusikia msimamo wake. Jambo la kwanza ni suala la Muungano na hasa nafasi ya Zanzibar kama ni "nchi au si nchi" na jambo la pili hatua zilizochukuliwa dhidi ya mafisadi wa EPA.

Suala la Zanzibar Rais Kikwete alisisita kuwa nchi yetu ni moja yanapokuja maswala ya nje lakini mambo yetu yenyewe "nchi ni Zanzibar, nchi ni Tanganyika".

Na kuhusu suala la EPA na maamuzi ya kuongeza muda kwa watu walioiba fedha hizo kuzirudisha na wasipozirudisha ndio watafikishwa mahakamani inaonekana nalo limepokelewa kwa hisia tofauti vile vilei.

Kwa vyovyote vile hotuba ya Rais inaonekana imeendelea kuwagawa Wananchi na kuzua maswali mengine zaidi ambayo ma-

NGUVU ZA HOJA

TUJIFUNZE KUWAKATALIA WATAWALA

Na. B. Mwalukasa

Wiki si nyingi zilizopita Waziri wa Nishati na Madini Bw. Wiliiam Ngeleja (pichani) alijikuta anakimbiwa na wasikilizaji wake wakati wa ufunguzi wa Semina mojawapo ya mambo ya madini huko Mpwapwa, Dodoma.

Wasikilizaji hao ambao ni wananchi kutoka Korea waliamua kutoka wakati Waziri anazungumza aidha kwa kuwa walichoka, au walikuwa hawajali kilichokuwa kinazungumzwa kwani hiyo ilikuwa ni semina iliyoandaliwa na CCM.

Mara baada ya kumaliza hotuba yake aliamua kuomba kipaza sauti na kumwagiza Katibu wa CCM wa Wilaya hiyo Bw. Deogratius Rutta kwenda nje kuwatafuta Wakorea hao na kuwarudisha ukumbini. Bw. Ngeleja aliamua "kuwapaka" hao kwa kuonesha dharau kwake.

Kimsingi Bw. Ngeleja kama walivyo viongozi wengine wanafikiri wananchi wanalazimika kuwasikiliza. Wanaamini wananchi lazima wawasikiliza lakini pia hata wageni wanalazimika kuwasikiliza.

Hili si kweli.



Kitendo cha Wakorea kuondoka ukumbini kwa sababu yoyote ile ilikuwa ni haki yao ya kujieleza na kutoa maoni. Haki hii haiitaji kibali cha Ngeleja.

Walichofanya Wakorea hao ni kuonesha kuwa wakati mwingine viongozi wakirudia porojo au maneno ya kisiasa jukwaani wananchi wana haki ya kuondoka hapo bila hata kuaga.

Haki hii na wajibu huu wa mtu kufuata dhamira yake na wito wa moyo wako haiji kwa sababu kina "Ngeleja" wanaitoa bali ni haki ya msingi ya utu wa mwanadamu.

Tukituambua wajibu huu kwetu wenyewe na kwa dhamira zetu hatuna budi kuwaonesha watawala wetu na viongozi wengine kuwa hatuwezi tena kuvumilia kusikiliza porojo na maagizo yasiyo na msingi wowote wa kisheria.

Jamii za wenzetu zilizoendelea katika utawala wa Kidemokrasia na sheria zimeweza kufanya hivyo pale raia wake walipoweza kuwakatalia watawala wao na viongozi wao nguvu na mamlaka ambayo hawana kisheria. Hilo limefanywa kwa kuwapinga kwa kutumia kalamu, mihadhara ya hoja, maandamano n.k Lakini njia ambayo inatumiwa na wengi ni kuweza kumkatalia kiongozi kwa heshima zote na taadhima jambo ambalo hana nguvu kuamuru.

Kwa hapa Tanzania kuna viongozi (kama Ngeleja) ambao wanaamini neno lao ni amri na kwa vile wana vibendera na vimulimuli basi ni lazima kuwatii.

Kila raia utii wake wa kwanza kabisa kama mwananchi ni kwa sheria za nchi; na pale ambapo sheria ina utaa au hana uhakika wa sheria hiyo basi ni wajibu wake kuitii dhamira yake kwani hiyo ndiyo itakayomhukumu kwa haki.

Kumtii kiongozi kwa jambo ambalo lina utata wa kisheria au linapingana na dhamira yako ndio mwanzo wa kuwaacha waovu watawale. Tujifunze kukataa. Uovu haupingwi kwa kukaa kimya bali kwa kukataa wazi wazi.

MPANGO HUU UNATUDHALILISHA

Na. Jessica Leonard Fundi

Rais Kikwete ni mahiri sana wa maneno na anajua nini cha kusema hasa kwa sisi kina dada kiasi kwamba tunajikuta tunapiga vigelegele vya shangwe kwani anakuwa ametukuna roho zetu.

Alipozungumza na Wabunge siku ya Alhamisi iliyopita alisema kitu kimoja ambacho mwanzoni niliona ni kizuri lakini baada ya kufikiria sana nikaona ni kitu ambacho kinaendeleza mawazo ya mfumo dume kuwa wanawake wanahitaji kuonewa huruma na kupendelewa linapokuja suala la kupewa vyeo au kushika nafasi mbalimbali za uongozi.

Nikubali na kumpongeza Rais kwa kukusudia kuanzisha mchakato utakaowezesha nchi yetu kuwa na uwakilishi wa 50/50 Bungeni. Tukifika huko tutakuwa kweli tumejenga jamii yenye nafasi sawa kwa kila mtu. Tatizo langu kubwa ni kuwa katika kufikia lengo hilo au kwa kutumia mchakato huo watanzania wote tupewe nafasi sawa ya kupata nafasi badala ya kutoa upendeleo au kufanyiwa huruma.

Nasema hivi kwa sababu Rais katika hotuba yake alisema kuwa yeye akipewa majina ya watu ili ateua mmoja wao kushika nafasi fulani basi akiona jina la mwanamke



humo atatafuta "kila sababu" ili amteue mwanamke huyo. Hofu yangu ni kuwa katika kila hizo "sababu" atatumia jinsia.

Ni matumaini yangu kuwa Rais atakapomteua mwanamke yeyote kushika nafasi ya uongozi iwe ni kwa sababu mwanamke huyo anastahili, ana uwezo, na ni mtu ambaye anaiweza nafasi hiyo kutokana na uzoefu, elimu, na ujuzi wake. Mwanamke asipewe upendeleo kwa sababu ni mwanamke. Huu ni udhalilishaji na kutufanya tuonekane duni na tunausubiri vyeo vya upendeleo.

Kama bado tunakiri kuwa Binadamu wote ni sawa na mwanamke ni binadamu basin a yeye ni sawa na mwanadamu yeyote yule. Na kama bado tunaamini kuwa kila "mtu ana haki ya kuthaminiwa na kutambuliwa utu wake" basi mwanamke naye kwa vile ni mtu anastahili haki hiyo.

Mawazo haya ya mfumo dume lazima tuyapinge na kuyakataa hata kama yanatoka kwa Rais. Mwanamke kama ana uwezo, ujuzi, nia, elimu na nafasi ya kupewa uongozi basi apewe kwa sababu hizo na orodha isiangaliwe kama kuna Mwajuma au Helena ndani yake.

Soma bure

MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...


Picha ya Wiki




Rais Kikwete alipopokea ripoti ya Timu ya Mwanyika kuhusu uchunguzi wa wizi wa EPA. Ametoa siku 71 fedha zirudishwe au mahakamani

KATUNI ZA WIKI







KUTOKA KWENYE MTANDAO

HOTUBA YA RAIS

Hizo hela mmeshaambiwa sio za serikali, Serikali imeziweka chini yake sasa hivi. Kikwete kawanyamazisha sana kwani Ushindi 2010 pale pale. Na kina Slaa wakiongea zaidi keshawapa warning in a joking way so poleni tafuteni lingine. – **Sizzla**

Wataalamu fulani wanasema kwa dakika 10 za mwanzo unaihutubia hadhira yako. Dakika 10 zinazofuata unajihutubia mwenyewe. Baada ya hapo unamhutubia shetani. Akina Salva na Januari hawamshauri au kumwelimisha JK juu ya ufundi wa hotuba – **Invincible**

Mkuu alikuwa amepania kuvunja rekodi ya Komredo Kastro ila alilazimika kutomaliza hotuba yake. – **Companero**

Katika hotuba kikwete ameanzisha mazoea mabaya sana, kuwa wezi wakiiba wanaweza kusamehewa kama wakipewa muda wakarudisha walichoiba. Bila woga ameweka mazoea haya ndani ya Bunge, Sasa wale wezi waliovunja benki ya NBC, kwa mtindo huu warudishe yale mamilioni na kesi dismissed? – **Mwikimbi**

Benki Kuu yeye, Richmond yeye, mikoa yeye, Muafaka yeye, Madini yeye, Mchuchuma na mchuchumaaa yeye, umeme na walaji wa TANESCO yeye, na MICHEZO yeye. Hao mawaziri wake wanafanya nini yarabi? Hao wakuu wake wa mikoa wanafanya nini yarabi! mtu mmoja hawezi kufanya kila kitu!– **Mwalimu Jr**

Habari ndio hiyo. Usinione naendesha shangingi langu na kuishi kwenye jumba kubwa la ghorofa, serikali imevizuia vyote hivyo nina hali ngumu kweli.– **Fisadi Mdogo**

Kwa hiyo unatuambiaje?ungekua unakosoa pande zote mbili ningekuona mwanademokrasia,mbona kwa Mbowe hukuongea chchote au yeye sio fisadi? umepitwa na wakati mwkjj,sipendi mafisadi iwe ndani au nje ya ccm—**Kheri**

Cheche za Fikra
Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Ansbert Ngurumo—Makala

Jeffrey Msangi—Makala
Kwa kujiandikisha, maoni, habari, na ushauri

Tuandikie: Mhariri@klhnews.com

***Kanusho:** Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.*